

## ATHARI YA SANAA ZA MAONYESHO KATIKA JAMII

Mwanakombo Noordin

Chuo Kikuu cha Moi

### **Ikisiri**

Sanaa za maonyesho hujumlisha ngoma za kienyeji, muziki, densi, maonyesho ya jukwaa na mengineyo ambayo humhitaji mtu aonyeshe matendo fulani mbele ya hadhira. Sanaa za maonyesho hutofautishwa na sanaa nyengine kwa kuzingatia kipengele cha utendaji. Kila onyesho humlazimu mhusika ajibadilishe kisura, kivazi na kisauti kwa kutumia rangi maalum na vifaa vya sauti. Onyesho lolote lile huwa na mazungumzo, ishara za nyuso pamoja na za mikono, sauti za muziki au za wanyama, mandhari maalum na wahusika. Tunapochunguza athari za sanaa za maonyesho katika jamii, tunatathmini athari hizo na mchango wake katika nchi yetu. Athari hizo zinaweza kuelezewa kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Nafasi yake pia inaonekana katika maisha ya watu binafsi na katika maendeleo ya taasisi mbalimbali nchini. Je, kuna mbinu yeyote tunayoweza kuitumia kupimia athari za sanaa za maonyesho katika jamii? Katika makala hii, tutachunguza vipengele mbali mbali vinavyozingatiwa katika kulijibu swala hili. Pili, tutafafanua taratibu zinazozalisha athari hizo kwa kujadili nadharia anuai zinazotumika kufanikisha mjadala huu. Tatu, tutazishughulikia mbinu za uchanganuzi wa data na kuhitimisha kwa kutathmini mustakabali wa sanaa za maonyesho nchini.